





Neno	Maana	Picha
<p>Kifaa Saidizi cha kusikia</p>	<p>Hiki ni kifaa Saidizi cha kusikia kinachowekwa nyuma ya sikio ambacho kinaninginizwa juu ya sikio na kinakuwa nyuma ya sikio. Kuna kifaa kinachounganisha kisaidizi na kifaa kingine kiitwacho ‘ earmold” ambacho kinaungana na sehemu ya ndani ya sikio</p>	
<p>Katheta</p>	<p>Hiki ni kifaa laini kinachotumika kutoa mkojo nje ya kibofu cha mkojo cha mgonjwa. Kinatumika na watu ambao hawawezi kutoa mkojo kutoka kwenye vibofu vyao vya mkojo bila kupata msaada au pale wanapohitaji kufanya hivyo.</p>	
<p>Udhaifu wa mwili</p>	<p>Huku ni kukosa nguvu, ni hali ya kuweza kuathirika kwa urahisi au kuwa na nguvu kidogo. Mara nyingi hali hii hutokea pale watu wanapozeeka na hali ya afya yao kushuka.</p>	
<p>Kutokuwa na uwezo wa kuzuia mkojo-incontinence</p>	<p>Ni pale mtu anapopata ugumu au anapokosa uwezo wa kuzuia mkojo</p>	
<p>Saa ya mkononi inayotoa sauti</p>	<p>Ni saa ambayo ikiguswa inayotoa sauti kwa kutaja muda wa wakati huo</p>	
<p>Wafanyakazi</p>	<p>Watu wanaotua huduma fulani au wanaofanya kazi kwenye taasisi.</p>	
<p>Rolata</p>	<p>Ni kifaa cha kutembelea chenye matairi manne.</p>	
<p>Kiharusi</p>	<p>Hii hutokea pale ambapo damu inashindwa kufika kwenye ubongo. Hii inaweza kusababisha upande mmoja wa mwili kuwa dhaifu au kupooza, pamoja na matatizo mengine kwenye kuongea, kuhisi, kufikiria na kuona.</p>	

<p>Orodha ya vifaa sadizi vinavyopewa kipaumbele na Shirika la Afya Duniani</p>	<p>Orodha ya vifaa saidizi ambayo iliasisiwa na Shirika la Afya Duniani. Orodha hii inaweza kutumiwa na nchi husika kutengeneza orodha yake ya vifaa saidizi</p>	
<p>Mtindio wa Ubongo</p>	<p>Ni hali inayoathiri kutembelea, uwezo wa misuli kufanya kazi, utimamu wa mwili na ukaaji. Mtindio wa Ubongo ni matokeo ya ubongo kuathirika kabla, wakati au baada ya kuzaliwa.</p>	
<p>Down syndrome</p>	<p>Ni hali ambayo mtu anaweza kuzaliwa nayo. Down syndrome inaweza kuathiri afya, ukuaji na uwezo wa kufikiri. Watu wenye Down syndrome wanaweza kuwa na athari za kimaumbile.</p>	
<p>Kuumia kwa Uti wa mgongo</p>	<p>Mara nyingi Uti wa mgongo waweza kutokea kutokana na ajali au Ugonjwa. Baada ya Uti wa mgongo kuumia, taarifa haziweza kusafiri kutoka sehemu moja ya mwili hadi kwenda kwenye Ubongo. Mara nyingi mtu haweza kusogea (amepooza) na wala hawezi kuhisi chochote sehemu ya chini ya eneo lililoumia</p>	